



P.O.BOX 42983, MABATINI RD - DAR ES SALAAM

Website: www.ladiesinislamtz.or.tz

Email: info@ladiesinislamtz.or.tz / ladiesinislamtz@gmail.com

Phone: +255717250550 / +255744037033



TAARIFA KWA UMMA FURSA YA UDHAMINI WA MASOMO KWA WANAFUNZI WA KIDATO CHA SITA NA KOZI YA UUGUZI NA UKUNGA (2026/2027)

Assalaamu Alaykum Warahmatullahi Wabarakatuh!

Taasisi ya **Ladies in Islam Tanzania** kwa kushirikiana na taasisi ya **World Islamic Propagation and Humanitarian Services (WIPAHS)** inapenda kuutaarifu umma kuhusu fursa ya udhamini wa masomo kwa wanafunzi watakaokuwa wanaendelea na elimu katika mwaka wa masomo 2026/2027.

Fursa hii imetolewa na WIPAHS ikiwa ni sehemu ya jitihada zao za kuendeleza elimu na kuandaa viongozi bora wa baadaye kupitia msaada wa kielimu kwa vijana.

UDHAMINI UNAOTOLEWA:

1. Wanafunzi wa **Kidato cha Sita (A' Level)**: Wanafunzi 5 watapatiwa udhamini wa 100% ya ada ya masomo yenye jumla ya **Tsh 16,500,000** kwa muda wa miaka 2 ya masomo. Hivyo kila mwanafunzi atanufaika na kiasi cha **Tsh 3,300,000** kwa mwaka.

2. Wanafunzi wa Kozi ya Uuguzi na Ukunga; Wanafunzi 10 watapatiwa udhamini wa asilimia 100 ya ada ya masomo yenye jumla ya **Tsh 84,375,000** kwa muda wa miaka 2 ya masomo. Hivyo kila mwanafunzi atanufaika na kiasi cha **Tsh 8,437,500** kwa mwaka. Kwa mwaka wa masomo **2026/2027**, jumla ya wanafunzi 15 watanufaika na udhamini huu wenye thamani ya **Tsh 100,875,000**.

GHARAMA ZA MALAZI NA CHAKULA:

Kila mwanafunzi atalipa gharama za malazi na chakula ambazo ni Tsh **1,850,000** kwa muda wa miaka 2 ya masomo. Hata hivyo, taasisi itatoa punguzo maalum kama ifuatavyo:

- Punguzo la maalum kwa kila mwanafunzi: Tsh **480,000**
- Punguzo la ufaulu mzuri kwa mwanafunzi : Tsh **470,000**

Hivyo gharama ya mwisho ya malazi na chakula itakuwa takribani Tsh **900,000** kwa muda wa miaka 2 ya masomo, na inaweza kulipwa kwa awamu **5 za Tsh 180,000**.

MASHARTI YA KUOMBA:

- Mwombaji lazima awe amefaulu daraja la kwanza katika masomo ya sayansi.
- Awe ni Binti wa Kiislam
- Awe tayari kuendelea na masomo katika shule za **WIPAHS zilizopo Kibaha, KM 800** kutoka Morogoro Road.
- Awe na nidhamu, bidii na utayari wa kuendeleza elimu kwa manufaa ya jamii.

IKUMBUKWE:

WIPAHS ni taasisi kongwe yenye zaidi ya miaka 40 ya kutoa huduma katika sekta ya elimu kupitia shule zake pamoja na chuo cha **Wali U-Asr Education Centre** iliyopo Kibaha.

Kwa mwaka wa masomo 2026/2027, taasisi inatarajia kupokea wanafunzi wenye sifa stahiki ili kunufaika na udhamini huu muhimu wa kielimu.

Tunawahimiza wazazi, walezi na wanafunzi wenye sifa kutumia fursa hii adhimu kwa maendeleo ya elimu na mustakabali wa vijana wetu.

"Tumaini la Taifa ni vijana wake."

Kwa mawasiliano zaidi:

Simu: +255 744 037 033 / +255 683 786 313

Barua pepe: ladiesinislamtz@gmail.com / info@ladiesinislam.or.tz / info@wipahs.co.tz

Imetolewa na:

LADIES IN ISLAM TANZANIA

Kwa kushirikiana na

WORLD ISLAMIC PROPAGATION AND HUMANITARIAN SERVICES (WIPAHS)